MRADI WA JAMII YA WAFUGAJI WILAYA YA NGORONGORO

ERETO

RIPOTI YA KIJIJI CHA OLPIRO KUHUSU TATHMINI YA MAHITAJI YA JAMII YA WATATOGA NA JITIHADA ZAO ZA KUYATATUA: **7/10/2003**

YALIYOMO

1. **DIBAJI**
2. **UTANGULIZI**
3. **HISORIA YA KIJIJI CHA OLPIRO**
4. **RATIBA YA KAZI**
5. **KUTEMBELEA VITONGJI:** (1) **OLPIRO KATI**
   (2) **OLTOGOM**
   (3) **MUSHORJOGA**
6. **MAONI YA WAWEZESHAJI**

WAWEZESHAJI

1. JAMES MORINGE -AFISA MRADI ERETO, KATA YA ENDULEN
2. WILLIAM OLE NJOE -AFISA MRADI ERETO, KATA YA KAKESIO

UTANGULIZI

Katika utendaji wa kazi ya mradi ndani ya awamu ya pili ni kwanza kushirikiana na kusaidia jamii ya kifugaji ya WATATOGA, kati ya shughuli zake ni kuwanunulia mifugo watu maskini, pamoja na kutoa huduma kwa mifugo. Pamoja na kushughulikia swala la Gikaptha pia mradi ulichukua jukumu la kuwatuma maofisa wake wa mradi kutoka Kata mbili ambazo ni Endulen na Kakesio kutembelea Kijiji cha Olpiro kuanzia tarehe 7/10/2003.

Taarifa hii sehemu kubwa inaelezea jinsi mradi utakavyofanya kazi pamoja na wafugaji wa Kitatoga. Shughuli zenyewe za mradi ni kuanzia tarehe 30/6/2003 – 2008.

Wenyeji wa Olpiro wanapenda sana kufanya kazi na mradi ikimaanisha wafanyakazi wa mradi, ilianzia hasa hasa tarehe 23/9/2003 walipotembelewa na Meneja wa ERETO pamoja na Field Officer wa Kata ya Endulen. Siku hiyo walitupangia siku ya kwenda kuwaona ambayo ni tarehe 7/10/2003, na siku hiyo tulifika kama ilivyopangwa. Na wenyeji waliona faraja, mwanga, matumaini tulipoongea nao, kuhusiana na GIHAPTHA nia ambayo Watatoga walitumaini kuwasaidia maskini wao (ARBABAR).

Mradi hauna budi kusifiwa na jamii kwa kuwafikiria Watatoga kwa mara ya kwanza ya awamu ya pili wka kuwatuma wafanyakazi wa mradi.

Kwenda kutumia mbinu shirikishi ya kutenda kazi na jamii. Ndani ya ripoti hii ujuzi mwingi umetumika na jamii na utakutana na mbinu shirikishi zilizotumika na wenyeji katika kujitambua, kujieleza na kutenda. Safari hii ilianza 7/10/2003 – 10/10/2003, saa 10:25 na kufika Olpiro saa 7:00 mchana ambapo tulianza kazi na jamii baada ya mkutano mkuu wa Kijiji.

HISTORIA YA KIJIJI CHA OLPIRO

Mradi umeamua kwa awamu kuanzak ushirikiana na wafugaji wa Kitatoga wanaoishi ndani ya hifadhi ya Ngorongoro. Olpiro ni mojawapo ya vijiji vitatu vinavyounda Kata ya Endulen nazo ni:- Endulen, Esere na Olpiro. Vyote vikiwa ndani ya Tarafa ya Ngorongoro na ni mojawapo ya vijiji kumi na nne vilivyo andikishwa chini ya sheria ya Serikali za Mitaa, vile vile ina wajumbe wake ndani ya Baraza la Wafugaji. Kijiji hiki kina vitongoji vitatu navyo ni:-

(1) Olpiro kati
(2) Mushorjoga
(3) Oltogom

Kijiji cha Olpiro kiko kusini mwa makao makuu ya Kata, inayopakana na Kakesio upande wa magharibi kKata ya Oloirobi upande wa Mashariki, Kusini inapakana na Wilaya ya Karatu Tarafa ya Mang'ola. Kijiji cha Olpiro imetengwa kimaendeleo na kuonyesha kumegwa, kwani hakuna barabara ya kwenda ndani ya Tarafa. Maana yake iko chini ya mkia, bonde kubwa na hawajatengenezewa barabara. Wafanyakazi na wenyeji wote hawana mawasiliano na huko makao makuu ya Kata na hata Wilayani. Hivyo kibisashara vile vile hawana kipato kwani hwana njia ya kutokea zaidi ya kuswaga punda.

WAKAZI WA OLPIRO:
Jumla ya wakaazi wa Olpiro ni 2600 hii ni kwa mujibu wa sensa ya mwaka 1998.

Idadi ya	163
Ng'ombe	3000
Mbuzi	3000
Punda	1000

RAMANI YA KIJIJI CHA OLPIRO



MALENGO YA SAFARI YA OLPIRO:

1. Kuanza kushirikiana na jamii ya Kitatoga ambao ni wafugaji wa Tarafa ya Ngorongoro ndani ya NCA katika huduma za kijamii.

2. Kusaidia kuelewa mbinu/njia ambayo jamii hii ya kifugaji ya Kitatoga inatumia kusaidia watu wake walio maskini fukara ili kuwezesha mradi wa Ereto kuwasaidia wao kupitia njia zao za kimila na zinazokubalika na wao

3. Kuelewa mfumo wa jmaii ya Kitatoga kama wafugaji muundo wa jamii na majukumu ya vikundi na kuona ni jinsi gani mfumo huo wa maisha unaathiri masuala yahusuyo maendeleo yao ya kila siku.

4. Kusaidiana na jamii lengwa kupata majina idadi ya watu ambao ni maskini hasa kwa kutumia njia zao za kimila na desturi.

5. Kusaidia kufanikisha kuunda Kamati ya shughuli za mradi ili kuwezesha mradi wa jamii ya wafugaji- Ereto kuwafikia walengwa ndani ya jamii

6. Kupata majina ya jamii ya Kitatoga ya watu fukara ambao wamepata msaada toka kwa ndugu, jamaa na marafiki. Nia hasa ni kuona utaratibu mzima unavyofanyika na uwajibikaji wake kwa wanaosaidiwa

RATIBA YA KAZI:

TAREHE	KITONGOJI	KIKUNDI	MBINU SHIRIKISHI ZA PLA
7/10/2003	OLPIRO KATI	WANAWAKE & WANAUME	RAMANI, KALENDA MLINGANISHO NA UWEZO.
8/10/2003	MUSHORJOGA	WANAWAKE & WANAUME	MLINGANISHO, MUUNDO WA JAMII (CHAPATI)
10/10/2002	KIJIJI KIZIMA	WANAWAKE & WANAUME	TAARIFA YA KAZI
11/10/2003	KUWASILISHA TAARIFA KWA UONGOZI WA MRADI	WAWEZESHAJI	

WALIOHUDHURIA MKUTANO NA KUSHIRIKIANA NA WAFANYAKAZI WA MRADI WAERETO KIJIJI CHA OLPIRO KATI

Na.	Jina	Jinsia
1.	Nalida Ginanani	M
2.	Emilliana Rumay	F
3.	Christina Agustino	F
4.	Melwa Habujal	F
5.	Merultah Gidioni	F
6.	Mayhayebe Dottoh	F
7.	Dahangay Shapati	F
8.	Lelee Grigis	F
9.	Sharahandi Sainyinga	M
10.	Selesta Kidagily	M
11.	Udabeta Geyaru	F
12.	Gwaydamy Gishinge	M
13.	Gidagosenga Shingada	M
14.	Gichang Matofai	M
15.	Habada jarman	M

16.	Murasoda Majengi	M
17.	Gideoni Darabe	M
18.	Gidamaso Bushinge	M
19.	Gitigan Gichichi	M
20.	Gwaruda Gidameja	M
21.	Gidagijanga Hayaina	M
22.	Gidaruni Lohay	M
23.	Datu Suiya	M
24.	Gidamenya Gochalota	M
25.	Mahinda Msungu	M
26.	Heckoh Jichichi	M
27.	Gidagahiyiy Gidajur	M
28.	Gitajir Gritotosi	M
29.	Gisichwista Gidaguy	M
30.	Shabahandi Sainga	M
31.	Udagwalu pambatay	F

Kumbelea Kitongoji cha Olpiro

Baada ya kumaliza mkutano wa hadhara saa 7:00 alasiri tulikwenda kula na kurudi saa 8:00 mchana. Tuliweza kuwagawa wenyeji kwa makundi mawili kuendana na vitongoji. Kitongoji cha kwanza ni Olpiro Kati ambayo Ndugu William Ole Njoe aliongea na kundi la wazee na Ndugu James Moringe aliongea na kundi la wakinamana kwenye vikundi.

Tulitumia mbinu shirikishi ya kutenda (P.L.A.) kwa zana zifuatazo:- Ramani ili kuelewa eneo malisho, makazi mito ndani ya Kijiji. Majina ya mwaka ni zana ambayo imetuonyesha matumizi, mahitaji uhamaji, neema kwa mwaka mzima, pamoja na mlipuko wa magonjwa. Zana nyingine ni matukio ya kihistoria kwa miaka saba (7) kuonyesha magonjwa ya mifugo kuwepo kwa majani, mvua.

Zana nyingine ni ya kiangazi kuonyesha shughuli na wajibu wake, hii inasaidia kuelewa kwamba kumhitaji kama mtu wa kuja kuelezea mambo ya maendeleo utampataje. Tumeuliza pia maswali na kutengeneza jedwali la mlinganisho wa uwezo/tajiri katika jamii yao.

JEDWALI KUONYESHA MLINGANISHO WA UWEZO

TAJIRI KULIKO	TAJIRI SANA	TAJIRI TU	KAWAIDA	MASKINI	MASKINI KIASI	MASKINI ZAIDI
200 – 300	100 – 150	40 – 100	15 – 30	5 – 15	Mbuzi 5 Ng'ombe 2	-
Hakuna mtu	1 Mtu mmoja	2 Watu wawili	2 Watu wawili	9 Watu tisa	24 Watu 24	

Kitongoji hiki kinaonyesha kwamba kina familia maskini 34.

1. NA SHIRIKISHI YA MAJIRA YA MWAKA

Zanahii ilionyesha kuwa ya mvuto kwa watumiaji wazee wa Kitongoji cha Olpiro Kati, kwani wazee waliweza kupanga miezi yote ya mwaka kwa kutumia lugha yao,

na tulikubaliana vitu vya kutumia mbavyo ni vya kawaida kama vile matunda ya miti na fedha kuonyesha. Mavi ya mbuzi, kondoo, kuonyesha malisho. Matawi ya miti kuonyesha mvua. Miti midogo mikavu kuonyesha njaa. Kwak utumia zana hii wazee waliweza kuonyesha vitu vingi ndani ya jedwali moja, mfano wingi wa maji, magonjwa ya mifugo, kuwepo kwa malisho, madawa ya mifugo nyakati za njaa, mavuno ya mifugo, mvua, bei ya mifugo.

MAJI:
Kijiji cha Olpiro hakina shida ya maji huwa na mito inayotitirika kwa majira yote ya mwaka, maji ya bomba yanapatikana.

MAGONJWA YA MIFUGO:
Kuendana na zana ya majira ya mwaka ya magonjwa mwezi wa mlipuko kuanzia mwezi wa tano (5) hadi mwezi wa kumi na mbili isipokuwa kuanzia mwezi wa kwanza hadi wa nne hakuna magonjwa.

MALISHO
Tuonavyo kwenye jedwali la majira ya mwaka kuwepo kwa malisho ni mwezi Januari hadi mwezi Juni. Kuanzia mwezi wa saba hadi kumi na mbili Kijiji hakina malisho, bali mifugo wanahama kwenda maeneo ya juu ya mlima Orbili ambayo ni eneo la Kijiji cha Esere.

MATUMIZI YA MADAWA
Madawa ya mifugo huanza kutumika mwezi wa tano, hasa pale panapokuwepo majani mengi, kupe huongezeka na kusababisha ugonjwa wa ndigana kali. Ugonjwa wa ndorobo unakuwepo kila wakati wa mwaka.

2. NJAA:
Njaa huanza mwezi wa tisa hadi wa kumi na mbili. Mifugo hudhoofika kwa miezi hii, hakuna jinsi ya kuchinja kwa udhoofu na hata kupeleka mnadani kuuza bei inashuka sana.

KUVUNA MIFUGO
Mwezi wa sita na wa saba ni miezi ambayo inafaa kwa kuvuna mifugo hii inatokana na mifugo wengi na hali (afya) nzuri, na bei ya mifugo kwenye minada inapanda sana.

MVUA
Katika eneo zima la Olpiro mvua huanza mwezi wa kumi na mbili hadi mwezi wa nne, hivyo miezi ya pili na watatu ni miezi ya mvua kubwa sana.

3. MASWALI YALIYOULIZWA NA KIKUNDI CHA WANAWAKE OLPIRO KATI

GIHAPTHA MAANA YAKE NINI?
Ni njia ambayo jamii ya Kitatoga inatumia kuwasaidia ndugu/jamaa/marafiki wao maskini.

- Aliyeishiwa na mifugo huitwa ARBARBAR anachangiwa.
- Aliyeibiwa mifugo anachangiwa.

- Mama mjane mwenye watoto wadogo aliyeachwa bila mifugo anachangiwa.
- Boma inapoungua hutolewa msaada.

NI VITU KIASI GANI HUTOLEWA KAMA GIHAPTHA?

Mchango unaotolewa hauna kiwango bali hutegemea na uwezo, moyo wa anayechangia.

- Kwa maskini walioishiwa na mifugo, basi huchangiwa mifugo ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda.
- Kwa aliyepata ajali ya moto kuchoma boma, atachingiwa vilivyoungua humo bomani, vyombo, mbuzi, unga n.k.

NI KIASI GANI CHA MIFUGO HUTOLEWA KWA ANAYEPEWA GIHAPTHA?

Ni kiasi chochote

- Inaweza kuwa ng'ombe 1, 2, 3
- Inaweza kuwa mbuzi 1, 2, 3, 4, 5 – 10
- Inaweza kuwa kondoo 1, 2, 3, 4, 5 – 10
- Inaweza kuwa punda 1 – 3

ZANA SHIRIKISHI YA MATUMIZI YA MUDA WA MAMA WA KITATOGA WAKATI WA KIANGAZI

11:00 Asubuhi	Anaamka
11:05 – 1:15	Kusaga mahindi kwa kutumia jiwe
1:15 – 1:30	Kuchota maji
1:30 – 2:30	Kupika
2:30 – 3:00	Kufungulia mifugo kwa malisho
3:00 – 3:15	Chakula kwa wanaokwenda kuchunga
3:15	Chakula kwa Mzee
3:20 – 6:00	Shambani
6:00	Chakula kwa Mama na watoto
6:15 – 8:30	Kupumzika, kushona shanga
8:30 – 9:45	Kurudi shambani
10:00 – 10:30	Kuni
10:30 – 11:00	Kutengeneza vibuyu
11:15 – 12:00	Mifugo kurudi na kuangalia
12:15 – 1:00	Kukamua
1:15 – 2:00	Kupika, kulisha watu wote
2:00 – 2:15	Kuchekecha maziwa
2:15 – 3:00	Kukusanyika kuimba
3:15	Kukusanya ndama kupeleka ndani
4:00	Kulala

RATIBA YA MAMA WA KITATOGA WAKATI WA MASIKA

11:00 Asubuhi	Kuamka na kuchekecha maziwa
12:00	Kutayarisha vibuyu
12:30	Kusaga unga
1:00	Kufagia

1:30	Shamba
2:00	Shamba
3:00 – 5:00	Kukamua
5:00	Kupika
5:30	Kulisha watoto
6:00	Kuchagua ndama
7:00 – 9:00	Kushona shanga
10:00	Shamba
11:00	Kuni
12:00	Kutayarisha vibuyu
12:30	Mifugo kurudi nyumbani
12:35 – 2:00	Kukamua
3:00 – 4:00	Kuimba
4:30	Kuchagua ndama
5:00	Kulala

ZANA SHIRIKISHI YA HISTORIA YA MATUKIO 7/10/2003

Imechorwa na Wazee wa Olpiro Kati kuonyesha vitu/matukio yaliyojiri ndani ya kijiji cha Olpiro kwa miaka saba. Waliweza kuonyesha magonjwa ya mifugo ukubwa wake ndani ya miaka iliyotakiwa, kama vile upatikanaji wa malisho, kuwepo kwa mvua kwa miaka hiyo.

Angalia Jedwali hilo (HISTORICAL PIES)



KUTEMBELEA KITONGOJI CHA OLDOGOM 8/10/2003

Kama ilivyokuwa katika Kitongoji kilichotangulia cha Olpiro Kati, kitongoji hiki tuliweza kukutana nao, na walitukaribisha vyema.

"Walituchinjia mbuzi mmoja na vinywaji baridi tulivipata, na tunawashukuru kwa ukarimu wao".

Shughuli tuliyoanza ni kwa kutuambia mbinu shirikishi za kutenda kwa pamoja nayo ni mchoro wa chapati. Tuliwagawa vikundi vitatu na James Moringe alichukua kikundi cha Wazee na Ndugu William Ole Njoye alichukuwa kikundi cha wanawake.

Wazee waliweza kutuelezea kwa mchoro jinsi majukumu ya jamii yao yanavyokwenda. Angalia mchoro wa Jedwali la Chapati.



(1) MANYENDAH:
Ni Mtabiri

(2) GAHEDASENGA:
Mti baridi
Mtu apelekaye ujumbe kwa jambii toka Manyendah.

(3) GWARGWE
Mzee wa Kimang'ati

(4) ARGWEJAN:
Wakina Mama

(5) SIGOCHAND HAWEEGA:
Kiongozi wa Vijana wa kiume

(6) SIGOCHAND HARREMANGA:
Kiongozi wa Vijana wasichana.

ZANA SHIRIKISHI RAMANI: 7.10.03

RAMANI YA KIJIJI CHA OLPIRO

Imechorwa na Wazee wa Kitongoji cha Olpiro Kati



ZANA SHIRIKISHI YA MAJIRA YA MWAKA

Imechorwa na Kundi la Wazee Olpiro Kati 7/10/2003



Jamii ya Kina Mama wa Kitatoga walifanikisha pia kutuonyesha mgawanyo wao wa jinsia ulivyo. Hawa ni Akina Mama wa Kitongoji cha Olpiro Kati.

MGAWANYO KUNDI
LA WANAUME

BALOOJ
Hawa ni vijana wadogo
wanaochunga ndama

ARREMAY
Ni Morani wa Kitatoga
ambao hulinda jamii.

BILETIHANET
Ni vijana wakubwa walio
kuwa na wake tayari na
Waangalizi wa amani.

GWARWE
Wakubwa ambao wao hutoa
Maagizo ya kutekelezwa
kwa vijana wakubwa.

MGAWANYO WA KUNDI
LA WANAWAKE

HAWEET
Hawa ni wasichana
waliokwisha balehendama.

MARWEJAN
Ni wasichana ambao
tayari wameshachumbiwa

SIBEEDAN
Wanawake wenye watoto
wawili hadi wanne.

HAQKNODIK
Wakina Mama Wazee

Tarehe 8/10/2003

Waliohudhuria mkutano wakishirikiana na wafanyakazi wa Mradi wa ERETO Kijiji cha Oldogomsha

NA.	JINA	JINSI
1.	Lengai Engisich	M
2.	Agustino Rumay	M
3.	Gidamengi Gufonjoda	M
4.	Gidamani Sendema	M
5.	Gangaro Shingida	M
6.	Gatebeka Ginada	M
7.	Gidaghesenga Gidarosta	M

8.	Baruyeda Gebeja	M
9.	Gidahugua Qambaday	M
10.	Ghafani Gidorigi	M
11.	Silewista Hurba	M
12.	Gabaka Guduru	M
13.	Gerabasta Gituru	M
14.	Motrais Hirba	M
15.	Gidebosta Giocaruda	M
16.	Gidamangarza Gerebasta	M
17.	Gwaidesh Gidashingado	M
18.	Gidagebudi Gisiruda	M
19.	Hilonga Gwaruda	M
20.	Gituru Gingongi	M
21.	Daletari Lekwahay	M
22.	Gitambo Nanagi	M
23.	Gichemshi Hirba	M

WALIOHUDHURIA MKUTANO WAKISHIRIKIANA NA WAFANYAKAZI WA MRADI WA ERETO KIJIJI CHJA OLDOEION

NA.	JINA	JINSIA
1.	Lelee Girrigisich	F
2.	Mama Mariamu	F
3.	Mama Baiki	F
4.	Adamejara Gridobat	F
5.	Udabakari Nanagi	F
6.	Mama Jotoashi	F
7.	Ujala Gwaruda	F
8.	Udenda Gidot	F
9.	Udagawisch Gidagawibudi	F
10.	Udagerabasta Sichwista	F
11.	Mama Kwelu	F
12.	Udamudidi Gidarosta	F
13.	Udangwajeda Gidawalwel	F
14.	Mama Mitagas	F
15.	Udamishay Gidahuida	F
16.	Mama Uchera	F
17.	Mama Gabala	F
18.	Udageyau Gidion	F
19.	Udagordaga Gidabolida	F
20.	Utuwi Mengera	F

Wazee wa Kitongoji cha Oldogom waliweza pia kutueleza wajibu wa mzee wa Kitatoga kuanzia asubuhi hadi jioni.

Wakati wa kiangazi angalia jedwali al kiangazi:-

9:00 alfajiri Kuamka kuangalia kama ng'ombe wote wapo salama na kubaki nje ya boma.

9:30	Kuamsha mama na watoto
10:00	Ng'ombe kukamuliwa
10:30 – 11:00	Kuchaguliwa ndama yeye anakula tayari kwa kutoa ng'ombe.
12:00 – 2:00	Kutoa nd'ombe kusindikiza malishoni na kurudi.
3:00 – 5:00	Kutoa mbuzi na ndama kupeleka maji na kubaki huko kwa masaa.
6:00 – 9:00	Kula na kupumzika
10:00 – 11:00	Kwendak upokea mbuzi
12:00 – 2:00	Kukutana na ng'ombe (kupokea)
2:00 – 3:00	Kushika ng'ombe ambaye hapenda ndama kunyonyesha ndama – kufunga kamba.
3:00 – 5:00	Wazee kupumzika kulala
5:00 – 8:00 usiku	Unalal kidogo, unaamka kukaa nje ili kuangalia ng'ombe goigoi.

Oldogom

Jedwali la Masika: Wazee wa Kitatoga

9:00	Asubuhi kuamka. Kuamsha mama watoto wafungulie ng'ombe kwenda nje – sababu ya matope.
10:00 – 12:00	Kukaaa na ng'ombe nje ya boma.
12:15 – 4:00	Kupeleka ng'ombe malisho ya muda kabla ya kukamuliwa.
4:00	Kurudisha ng'ombe nymbani kukamuliwa.
6:00	Mzee kupata chakula
6:30 – 12:00	Mapumziko ya Mzee
12:15 – Jioni	Kurudi ng'ombe na kubaki nje ya boma.
3:00	Kurudisha ng'ombe ndani ya boma na kuchaguwa ndama, ndani ya ng'ombe.
4:00	Kula chakula na kupumzika.
6:00	Utaamka kuangalia ng'ombe walioanguka ndani ya matope bomani au kuzidiwa nguvu na wenzao.

Katika Kitongoji cha oltogom kazi yetu kubwa nyingine ilikuwa ni kupata majina ya watu maskini ambao wamepata Gihaptah, na hata wale ambao bado.

Tuliuliza swali kwa makundi yote tuliyokutana nayo:
Sali: Mtu anayeitwa Maskini (Arbarbar) ni mtu wa namna gari?

- Ni mtu asiye kuwa na mifugo toka mwanzo.
- Ni mtu ambaye mifugo yake imekufa kwa magonjwa.
- Ni mtu ambaye aibiwa mifugo.
- Mtuasiyekuwa na watoto
- Mama ambaye mali imeisha na ana watoto.

Mtu aliye nafuu ni wa namna gani?

- Ni mtu ambaye ana mifugo wachache
- Ni mtu ambaye anahangaika kutafuta
- Ni mama ambaye ana ndugu wenye uwezo na binafsi yake hujihangaisha.

- NI mtu ambaye ana uhakika wa chakula.

Angalia Jedwali la Mlinganisho wa uwezo wa jamii hii:-

KITONGOJI CHA OLTOGOM

TAJIRI KULIKO	TAJIRI SANA	TAJIRI TU	KAWAIDA	MASKINI	MASKINI KIASI	MASKINI ZAIDI
Ng'ombe 200 – 300 Wanawake 10 Hakuna mtu	Ng'ombe 100 – 150 Hakuna mtu	Ng'ombe 40 – 100 Watu 1	Ng'ombe 15 – 30 Watu 5	Ng'ombe 5 – 15 Watu 5	Ng'ombe 2 Mbuzi 5 watu 28	Bila chochote ni watu 3

Jamii ya Kitatoga wanapokuwa ndani ya Boma wanaishi kwenye nyumba tofauti. Mama anaishi kwenye nyumba yake na watoto wa kike pamoja na wa kiume wenye chini ya umri wa miaka saba.

Baba huishi kwnye nyumba yke iitayo "HULLANDA" na watoto wa kiume wenye umri wa miaka 10 kwenda juu. Nyumba ya Baba ndiyo ya wwageni wote wajao kwenye boma na hawaruhusiwi kwenda kwa Mama, wataletewa chakula pamoja.

Angali jedwali la Boma ya Kitatoga:

Mtatoga kwa kawaida hawaishi ndani ya Boma zaidi ya familia mbili tofauti. Kijana akishaoa natengeneza boma lake.



Uongozi wa Mila ya Kitatoga

- GAHEDA SENGA (MTI BARIDI)
  Huyu ndiye msemaji mkuu wa shughuli za kimila ndani ya Watatoga. Kiongozi huyu huchukua maagizo toka kwa jamii na kupeleka kwa Manyendah, huitwa mkuu wa Wamang'ati anayeshughulikia matambiko.

- MANYENDAH:
  Huyu ni mtabiri wa Kitatoga, yeye hutoa maagizo kwa Gaheda Senga kuhusu nini kinapaswa kufanywa na jamii ya Kitatoga.

- SIGOCHAND HARREMANGA
  Huyu ni kiongozi wa vijana wa kiume wa Kitatoga (Wamorani) na anasimamia pia mambo ya wasichana kwa kuwasiliana na kiongozi wa wasichana – nachaguliwa na vijana.

- SIGUCHAND HAWEEGA:
  Anashughulika na maswala ya mila yahusuyo wasichana na kuwasiliana na kiongozi wa wavulana – anachaguliwa na wasichana.

Nilijaribu kuwapata hawa viongoi wa vijana wa jinsia zote lakini niliambiwa hawajulikani na wazee, ni vijna wenzao tu na hawatakiwi kujuliaknana.

GIHAPTAH INASIMAMAIWA NA NANI?

- Ukoo wa anayepewa mifugo.
- Shemeji
- Marafiki

Kwa wlae ambao walimaliza ng'ombe kwa kunywa, ng'ombe wao watasimamiwa na Serikali ya Kijiji. Hii ilitokana na kuonekana kwamba wengine wana wake na watoto hivyo wameona wakinamama ni muhimu kutunziwa watoto kwa kupewa Gihaptah.

Mtu aliyemaliza ng'ombe kwa pombe hapewi Gihaptah. Mtu aliyeacha ng'ombe wakafa kwa kukosa malisho hapewi Gihaptah.

Nani anapaswa kupata Gihaptah:

- Asiye na kipato (Arbarbar)
- Aliye na ng'ombe chache wasiotosheleza watoto
- Familia iliyoibiwa mifugo.
- Familia ambayo mifugo wameisha kwa magonjwa.
- Wajane walioachwa na waume bil mifugo.

Tarehe 8/10/2003

WALIOHUDHURIA MKUtano wakishirikiana na wafanyakazi wa mradi wa ereto kijiji cha mushorjock

NA.	JINA	JINSIA
1.	Gidagwanedi Waids	M

2.	Shilli Gidobat	M
3.	Muhindi Alio	M
4.	Ngangaya Matafani	M
5.	Masarja Lale	F
6.	Udamekwa haboju	F
7.	Usecheda Giyangida	F
8.	Udamuchu Nanids	F
9.	Udamahana Gisupt	F
10.	Yeyo Gidawas	F
11.	Udabunda Gishagwanga	F
12.	Zala Qan Musungu	F
13.	Saktaw Gidaguu	F
14.	Mama Lelelu	F
15.	Udarnasauna Ginini	F
16.	Mame Giarau	F
17.	Unan Mamoya	F
18.	Udagilega Gitonyoda	F
19.	Udashega Vululio	F
20.	Udamawas Giyaya	F
21.	Udanghega Gidaganga	F
22.	Usaluga Gitonyoda	F
23.	Udamisaneda maruhata	F
24.	Mama Qara Qara	F
25.	Mama lelilelu	F

Waliohudhuria mkutano kushirikiana na wafanyakazi wa mradi wa ereto kitongoji cha Mushorjoga

NA.	JINA	JINSIA
1.	Sharahadi Saiga	M
2.	Gidainyi Gidasisi	M
3.	Gitenyeda Gidaguy	M
4.	Jarumani Balawa	M
5.	Gishaini Gutida	M
6.	Udamalena Hhaboju-mke	F
7.	Udamalena Gisipot	M
8.	Gidamani Sendumwa	M
9.	Gafimani Gidanigi	M
10.	Bebaste Gutura	M
11.	Gidagewibudi Gisuruda	M
12.	Lele Girigish	F
13.	Upapa Ghagha	F
14.	Chiritina Rumay	M
15.	Udagawishi Gidawibudi	F
16.	Gidamtash Gechaned	M
17.	Jotoshi Gitinu	M
18.	Gabreli Loshoy	M
19.	Udamaibe Datu	F
20.	Udaoalio Uambaday	F
21.	Udagola Gidamasoke	F

22.	Udarere Gichangike	F

8/10/2003

WALIOHUDHURIA MKUTANO WAKISHIRIKIANA NA WAFANYAKAZI WA MRADI WA ERETO KIJIJI CHA MOSHORJOCK

NA.	JINA	JINSIA
1.	Gwandaja Musungu	M
2.	Gidainy Gidasisi	M
3.	Gara Zara Mufurda	M
4.	Gidamajoda Gidabati	M
5.	Qerabesta Ginanani	M
6.	Hogo Gidawas	M
7.	Shabandi Bashiae	M
8.	Ginyongi Gidawas	M
9.	Gidogaweda Musungu	M
10.	Gidabanga Btirru	M
11.	Gidasho Dagati	M
12.	Gisunguda Gidababu	M
13.	Marighan Girigisch	M
14.	Gitenyanda	M
15.	Nyanda Gidagurja	M
16.	Gidagay Lehway	M
17.	Gitonyoda Giyengida	M
18.	Zawacha Majongu	M
19.	Mangingi Ngandashengi	M
20.	Gidaforoyoda Giyengida	M
21.	Gidako Gishe	M
22.	Mahinda Gishinsuda	M
23.	Jichichi Basiqe	M
24.	Gidangayo Gisuput	M
25.	Gidaoesenga Qilidaberenga	M
26.	Gidabaso Shingadeda	M
27.	Jarumani Balawa	M
28.	Exweso Hurba	M
29.	Gidahamani Hirba	M

Kutembelea Kitongoji cha Mushorjock
Kitongoji hiki kilikuwa cha misho. Tuliweza kufanya kazi kubwa ya malinganisho wa uwezo wa kijamii. Kitongoji hiki kina watu wengi sana maskini kwani kina Kaya 76 ambazo wanahitaji kusaidiwa.

Baada ya kufanya zoezi hili la mlinganisho wa uwezo, tulihamia kwenye mkutano mkuu wa Kijiji.

Jedwali la mlingishao (Wellbeing ranking)

KITONGOJI CHA MUSHORGA

TAJIRI KULIKO	TAJIRI SANA	TAJIRI TU	KAWAIDA	MASKINI	MASKINI KIASI	MASKINI ZAIDI
Ngo;ombe 200 – 300 Hakuna mtu	Ng'ombe 100 – 150 Watu sita 6	Ng'ombe 40 – 100 Wati tisa 9	Ng'ombe 15 – 30 Watu ishirini na moja 21	Ng;ombe 5 – 15 Watu kumi na nane 18	Ng'ombe 2 Mbuzi 5 Watu kumi na nane 18	Hakuna kitu Watu tisa 9

MAONI TOKWA KWA WAWEZESHAJI:

- mbinu za PLA nim uhimu kutumika kwenye sehemu zingine ambazo mradi unaanza shughuli zake upya.
- Watatoga hawampi mtu yeyote asiye na watoto Gihaptah.
- Kazi nyingi iliongzeka tarehe tisa hasa kutokana na kutumia mbinu kuu muhimu ya mlinganisho kwa vitongoji vyote.
- Watotga wameomba wanunuliwe mbuzi katika majira yote ya mwaka.
- Jamii hii wamependekeza kwamba mifugo yao inunuliwe katika mnada ya Wialay ya Karatu na Mbulu pindi mvua inapoanza.
- Familia maskini zinazohitaji Gihaptah msaada wa mradi ni kama ifuatavyo:-

	WATU	NG'OMBE	MBUZI	KONDOO	PUNDA
OLPIRO KATI	34	106	128		
OLDOGOM	44	100	88	10	17
MUSHOROJOGA	76	155	169	20	1
JUMLA	154	355	297	30	18

Mfafnikio mengine/Malengo: Mwisho tuliyofikia ni;

1. Kupata majina ya familia ambazo tayari wamepata Gihapta.
2. Kuchagua Kamati ya Gihapta kama ifuatavyo: Wajumbe ni Mama mmoja, wazee watatu:

Sifa:

- Awe anapenda kujitolea
- Awe mwaminifu
- Wawili waelwe kusoma na kuandika
- Wawe wafugaji

Waliochaguliwa:

(1) Mzee Lengai Grigisch

(2) Mzee Gwandaja Gidamusungu
(3) Afisa wa Kijij Gidamange Gunjonjoda
(4) Mama Christiana A. Rumay

HIV/AIDS

Ni swala tulilouliza, hata hivyo inaonekana kuwa jami ya Kitatoga haielewi janga hili.